

## Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia

"Kampeni hii inalenga kutoa elimu na msaada wa kisheria kwa wananchi katika maeneo yao ya karibu kupitia mikusanyiko ya kijamii ikiwemo mitaa, vijiji na kata"

MAMA SAMIA Legal Aid Campaign

# Mgogoro wa ardhi watatuliwa, majirani wapatana

KAMPENI ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia imerejesha uhusiano wa majirani wawili, Esther Rodrick na Rajabu Sinafungo wa Mtaa wa Msigani baada ya mgogoro wa mipaka ya ardhi uliodumu kwa miaka saba kufikia kikomo.

Suluhu hiyo ilipatikana jana baada ya majirani hao kufikishwa kwenye kampeni hiyo katika ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Ubungo na mawakili waliokuwa wakitoa elimu ya masuala ya sheria katika kata za mkoa wa Dar es Salaam.

Akielezea chanzo cha mgogoro huo, Wakili kutoka Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Lusajo Mwakasege alisema mgogoro huo ulianzia pale Sinafungo alipomshtaki Esther katika Serikali ya Mtaa wa Msigani na baadaye Baraza la Kata ya Msigani, akidai amevamia eneo lake kwa kupanda miti ya michongoma iliyotumika kama uzio.

Alisema malalamiko yake yalihitaji Esther kuondoa michongoma hiyo na kujenga uzio wa matofali ambapo Esther hakutaka kushinikizwa na mtu kujenga uzio mapema kwa kuwa michongoma ni yake na ardhi ni yake.

Alibainisha kuwa awali mgogoro huo uliwahi kusuluhishwa na uongozi wa serikali za mitaa ambapo ilikubaliwa kuwa eneo la michongoma ni mali ya Esther.

Hata hivyo, kutokana na maua ya michongoma kuanguka upande wa Sinafungo, Esther alitakiwa kuiondoa michongoma hiyo na kujenga uzio wa matofali pindi atakapopata fedha.

Alisema cha kushangaza baada ya miezi miwili Sinafungo alifungua tena shauri katika Baraza la Kata, akikiuka makubaliano ya awali.

"Timu ya wanasheria kutoka Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ilichukua jukumu la kushughulikia malalamiko hayo. Tulimwita mwenyekiti wa mtaa, ambaye alithibitisha kuufahamu mgogoro huo na kushangazwa na hatua ya Sinafungo kuvunja makubaliano," alisema.

Alisema Juni 19, 2025 walifika eneo la mgogoro kujionea hali ilivyo na kubaini kuwa eneo la mgogoro lina upana wa takribani nusu meta na urefu wa takribani meta nane.

Alieleza kuwa baada ya majadiliano Sinafungo alikuwa akisisitiza kuwa eneo hilo ni lake na kukataa kusuluhishwa.

Mwakasege alisema jana wakiwa na maofisa ardhi waliwaita tena na kuwaelewesha vizuri. Sinafungo alielewa na kukiri kuwa eneo hilo lenye mgogoro si lake.

Alisema Sinafungo aliomba michongoma iondolewe kuzuia uchafuzi wa eneo lake pamoja na kukubali Esther aondoe michongoma na kujenga ukuta wa matofali pindi atakapopata fedha, hata kama itamchukua miaka mitatu.

Kwa upande wake, Esther alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutuma mawakili hao kushughulikia migogoro ya wananchi na kurudisha haki kwa usawa.

Naye Sinafungo alieleza kuwa mgogoro huo uliduma kwa muda mrefu kwa sababu alikuwa hana uelewa wa masuala ya kisheria, hivyo kupitia kampeni hiyo amepata elimu ya sheria ndiyo maana hata imekuwa rahisi mgogoro kuisha.



Ofisa Ardhi Mkuu wa Jiji la Dar es Salaam, Godfrey Mlotwa akimhudumia mwananchi, Anna Mwanjoka katika Kata ya Segerea, Ilala, Dar es Salaam jana. (Picha na Ikunda Erick).

# Mjane arudishiwa nyumba, ateuliwa msimamizi wa mirathi

TIMU ya Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia wilayani Ilala Dar es Salaam imefanikiwa kumrudisha mjane kwenye nyumba yake na mumewe aliyefariki dunia na kusimamia kikao cha ndugu kukaa kisha kumteua mjane huyo kuwa msimamizi wa mirathi.

Hatua hiyo imefikiwa wakati timu ya kampeni hiyo ikiendelea na kutoa huduma katika kata za Wilaya ya Ilala ikiwemo Msongola eneo la Yangeyange.

Akizungumzia hatua hiyo, mmoja wa mawakili wa timu hiyo anayeshughulikia mgogoro huo, Kapufi Ally alisema wiki iliyopita wakati wakiendelea na kutoa huduma kwa wananchi wa eneo hilo, mjane Mariam Julius alifika kulalamika ndugu wa mumewe wamemfukuza kwenye nyumba na wanataka kuuza nyumba hiyo bila kumshirikisha ilihali ana watoto wanaomtegemea.

Baada ya kusikiliza shauri hilo, ndugu wa mumewe walipata taarifa kuwa mjane huyo kapeleka malalamiko kwenye vyombo vya sheria na ndipo wakaitisha kikao na kumtaka aende.

Siku ya kikao mjane huyo aliwataarifu timu ya Mama Samia ya Msaada wa kisheria na kwenda nao na ndipo ndugu wa mume wakamwambia yeye si mke halali wa kaka yao kwa sababu alikuwa na mke mwingine baada ya kugombana na Mariam.

Kapufi aliingilia kati na kusema sheria ya ndoa haiko hivyo na kuwa ndoa ya kikristo ni ya mke mmoja na ili kuivunja lazima mahakama ihusishwe na talaka itolewe na kuwa kwa shauri la Mariam bado ni mke halali na anastahili haki zake kwenye nyumba hiyo.

Katika shauri hilo, mume ni Sammy Sezua na kuwa kaka yake aitwaye Wilfred ndiye aliyewaweka wapangaji kwenye nyumba ya mjane huyo na kuchukua kodi kwa madai kuwa familia imemteua asimamie, jambo ambalo si sawa kwani hakujafanywa kikao cha kuteua msimamizi wa mirathi.

"Tumeenda kwenye nyumba ya marehemu tumeshuhudia mke na watoto hawako hapo na nyumba imepangishwa kwa amri ya kaka (Wilfred) ambaye ndiye anapokea kodi na kuifanyia matumizi anayoyajua, huku mke (Mariam Julius) na watoto Sandry Sammy (13) na Sonia Sammy (10), wakiteseka na kukosa makazi," alisema Ally.

Awali timu hiyo ilifika nyumbani kwa marehemu na kushuhudia nyumba ikiwa na wapangaji wawili mmoja akilipa kodi ya Sh 80,000 kwa mwezi na mwingine Sh 60,000 ambazo wapangaji hao walikuwa wakimlipa Wilfred Sezua.

Wakati wapangaji wakisema hayo, Wilfred aliwaambia timu hiyo ya mawakili kuwa kodi anayochukua kwa wapangaji hao ni Sh 40,000 na 35,000 jambo ambalo wapangaji wamekana na kusema wanalipa Sh 80,000 na 60,000 kwa mwezi.

Baada ya sakata hilo, ndugu hao waliitwa na timu hiyo ya kampeni siku iliyofuata na kufanya kikao huku Wilfred akiwasilisha kibali cha mazishi na katika kikao hicho kikamteua mjane Mariam kuwa msimamizi wa mirathi.

"Tumesimamia kikao kimeenda vizuri na ndugu wameafikiana mjane Mariam awe msimamizi wa mirathi na tumewasadia kibali cha mazishi tukikiwasilisha Rita kwa ajili ya kupata cheti cha kifo ili mirathi ifunguliwe," alisema Ally.

Alisema kwa sasa wamefanikiwa pia kumrudisha mjane huyo kwenye nyum[illegible] na ndiye amekabidhiwa sasa asiman[illegible] wapangaji waliopo huko taratibu nyin[illegible] za mirathi zikiendelea.

# Msaada wa kisheria wamfichua baba mdhalilishaji

TIMU ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia imefanikisha kukamatwa na kushikiliwa kwa baba wa kufikia na Polisi wa Kituo cha Polisi Mwanagati, Kata ya Mzinga wilayani Ilala mkoani Dar es Salaam kwa tuhuma za kumfanyia unyanyasaji wa kijinsia mtoto wa mkewe huku akimtisha kuwa iwapo atasema anachomfanyia, atamwacha mama yake.

Akizungumzia tukio hilo, Wakili Kapufi Ally mmoja wa mawakili waliokutana na tukio hilo alisema wakati kampeni hiyo ikiendelea katika Kata ya Mzinga, Ilala walitembelea pia shule za msingi na sekondari kuwaelimisha wanafunzi na kuzungumza nao.

Ally alisema wakiwa kwenye shule moja ya msingi (jina linahifadhiwa) walipomaliza kuwaelimisha wanafunzi hao waliruhusu maswali na mahojiano kwa wanafunzi waliokuwa na maoni au jambo walilotaka kupata msaada.

"Alijitokeza mwanafunzi wa kike wa darasa la saba, analalamika baba yake (jina linahifadhiwa) wa kufikia anamfanyia ukatili na kumpa vitisho. Anasema wanaishi na baba huyo na mama yake mzazi na mama akiondoka baba anamwita na kumshika mikono yake miwili kwa nyuma huko mkono mmoja wa baba huyo ikimshika matiti na kuyapapasa," alisema.

Ally alisema mtoto huyo akikataa baba huyo wa kufikia anamtisha asiseme kwa mama wala kwa mtu yeyote na iwapo atasema mama yake ataachwa.

Alisema mtoto huyo amefanyiwa vitendo hivyo zaidi ya mara tatu lakini baba huyo hakufanikiwa kumuingilia kwa maana ya kumbaka.

Ally alisema baada ya kupokea malalamiko hayo waliomba ruhusa kwa mwalimu wa shule husika ili mtoto aende kuwaonesha timu hiyo nyumbani kwao na kumtambua mtuhumiwa na ndipo polisi waliokuwepo wakataarifiwa na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa na hadi sasa ameshikiliwa Kituo cha Polisi Mwanagati.

"Shauri liko polisi na uchunguzi unaendelea kwa sababu mtoto tulimpeleka hospitali ya serikali kufanyiwa uchunguzi zaidi na ukikamilika shauri litapelekwa mahakamani," alisema Ally.

Alisema mama mzazi wa mtoto huyo (jina linahifadhiwa) hakuwa anajua chochote kuhusu vitendo hivyo kwa mtoto wake na mtoto alizungumzia vitendo hivyo mbele ya timu hiyo na mama yake akiwepo ndipo aliposhtuka.

[illegible] vitendo hivyo alisisitiza kuwa [illegible] baba huyo au mtu mwingine na kuwa alichofanyiwa ni huo [illegible] wa baba yake huyo [illegible]

# Kampeni ya Samia yamrejeshea mama mtoto

**Na Ally Ruambo**

KAMPENI ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia (MSLAC) imemuwezesha, Johari Ally kurejeshewa mwanawe wa miaka miwili aliyenyang'anywa na ndugu wa mwanaume aliyezaa naye.

Johari amekabidhiwa mwanawe nyumbani kwake kupitia msaada alioupata katika banda la MSCAL katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yanayoendelea mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kufanikiwa kumrejesha mtoto kwa mama yake, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Haki za Binadamu, Beatrice Mpembo alisema kuwa haikua rahisi kufanikisha mtoto huyo kurejeshwa kwa mama yake kutokana na changamoto mbalimbali.

"Changamoto zilikuwepo lakini kwa kuzingatia sheria za nchi zinamtaka mtoto wa umri huo akae na mama na kama wataalamu tuliweza kushauri na kulifanikisha jambo hilo kwa amani," alisema.

Kwa upande wake, Johari aliishukuru serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuendesha Kampeni ya Msaada wa Kisheria iliyomsaidia kumrejesha mwanae.

Julai 10, mwaka huu Johari alifika katika banda la Wizara ya Katiba na Sheria akiwa anahitaji msaada wa kisheria wa namna ya kumpata mwanae aliyechukuliwa na ndugu wa baba yake kwa takribani miezi sita.

Baada ya kusikilizwa, wataalamu wa wizara waliweza kuwakutanisha mama wa mtoto na ndugu wa baba waliokuwa na mtoto ambapo walifanikiwa kumrejesha mtoto kwa mama yake na kuwashauri endapo watamuhitaji kwa ajili ya salamu wawasiliane na mama wa mtoto huyo.

Sambamba na Wizara ya Katiba na Sheria kutoa msaada wa kisheria pamoja na elimu ya sheria katika maonesho hayo pia wananchi wenye changamoto mbalimbali za kuhitaji msaada wa kisheria wametakiwa kuwasiliana na Wizara ya Katiba na Sheria kupitia kituo cha Huduma kwa Mteja kwa namba 0262160360.



**WANANCHI mbali mbali waliotembelea banda la wizara ya Katiba na Sheria wakipatiwa elimu inayohusu masuala ya sheria pamoja na msaada wa kisheria kwa wale wenye matatizo mbali mbali yanayohitaji msaada (NA MPIGA PICHA WETU).**

**HUKUMU**

# Mahakama Kuu yafafanua zuio viongozi wa CHADEMA

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam imetoa ufafanuzi wa zuio kwa wahusika 10 ambao hawatakiwi kushiriki katika shughuli zozote za kisiasa katika Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Watu hao waliozuiwa kutokana na kesi ya madai namba 8960/2025 iliyofunguliwa na aliyewahi kuwa Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Zanzibar, Said Issa Mohamed pamoja na Ahmed Rashid Khamis na Maulida Anna Komu.

Ufafanuzi huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na mawakili Gizo Simfukwe na Shaban Marijani, kutokana na taarifa zinazoendelea kuhusu zuio lililotolewa Juni 10, mwaka huu, kwa baadhi ya watu kujiondoa kwamba hawahusiki.

"Sisi kama wanasheria tunawawakilisha wateja wetu waliofungua kesi hii, tulimwandikia Msajili wa Mahakama Kuu Masjala Ndogo ya Dar es Salaam barua kuomba ufafanuzi wa kisheria kwamba je, lile zuio lililotolewa linawahusu kina nani,"alisema Wakili Simfukwe.

Alisema wamepokea barua ya majibu kutoka kwa Msajili ya Julai 14,225 ambayo hata wenzao wa upande wa pili wamepewa nakala ambapo baadhi ya watu walisema zuio ni la Bodi ya Wadhamini na Katibu Mkuu.

"Huu ndio ufafanuzi wa kisheria wa Msajili ameandika na kutoa kwamba hawa wote waliyotajwa hapa wamezuiwa hadi pale kesi ya msingi itakaposikilizwo na kutolewa uamuzi,"alisema.

> Sisi kama wanasheria tunawawakilisha wateja wetu waliofungua kesi hii, tulimwandikia Msajili wa Mahakama Kuu Masjala Ndogo ya Dar es Salaam barua kuomba ufafanuzi wa kisheria kwamba je, lile zuio lililotolewa linawahusu kina nani.
>
> **Wakili Gizo Simfukwe**

Wakili Simfukwe aliwataja watu hao kuwa ni Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Kaimu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Makamu Mwenyekiti CHADEMA Tanzania Bara au Kaimu Makamu Mwenyekiti CHADEMA Tanzania Bara.

Wengine ni Makamu Mwenyekiti CHADEMA Tanzania Zanzibar au Kaimu Makamu Mwenyekiti CHADEMA Tanzania Zanzibar, Katibu Mkuu CHADEMA au Kaimu Katibu Mkuu CHADEMA, Naibu Katibu Mkuu CHADEMA Tanzania Bara au Kaimu Naibu Katibu Mkuu CHADEMA Tanzania Bara, Naibu Katibu Mkuu CHADEMA Tanzania Zanzibar au Kaimu Na[illegible] Katibu Mkuu CHADEMA T[illegible]la Zanzibar.

Mbali na hao, wengine ni viongozi wote na katika ngazi zote wawe walioteuliwa moja kwa moja katika nafasi zao za uongozi au wanaokaimu na mfanyakazi, wakala au mtu yeyote anayefanya kazi hizo kwa niaba ya chama.

"Pia aliyepewa maelekezo au kuiwakilisha CHADEMA, atakayefanya kazi zozote za kisiasa kwa kutokea taifa, mkoa, wilaya, halmashauri, tarafa na maeneo yote nchini kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar,"alisema.

Wakili Simfukwe alisema madhara ya mtu atakayekwenda kinyume na uamuzi wa Mahakama atakuwa anatenda kosa la jinai, ambalo linajulikana na kudharau amri ya Mahakama na pia anaweza kuchukuliwa hatua zingine za kimadai kwa mujibu wa sheria.

"Kwa sababu Mahakama inapoelekeza na wewe ukaenda kinyume cha Mahakama kwa kujificha katika mwavuli kwamba "mimi hainihusu", huo utakuwa uvunjaji wa sheria. Tumeamua kutoa ufafanuzi huu kwa umma kuondoa upotoshaji kwa baadhi ya watu," alisema.

Wakili Marijani alisema watu hao waliotajwa hawatakiwi hata kuzungumza na vyombo vya habari kuhusiana na masuala ya chama.

Mahakama ilikubali maombi hayo na zuio lililotolewa kwa mujibu wa amri ya Jaji Hamidu Mwanga katika shauri dogo la madai namba 8960 la mwaka 2025 wakati uamuzi wa maombi katika kesi ya madai namba 8323/2025 likisubiriwa kutolewa uamuzi.

Scanned with [illegible] SCANNER

# Uamuzi maombi ya marejeo ya Lissu kutolewa Agosti 12

**Na Ramla Hamidu**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam Masijala Ndogo Agosti 12, mwaka huu inatarajiwa kutoa uamuzi wa maombi ya marejeo yaliyofunguliwa na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu dhidi ya upande wa jamhuri.

Jaji Elizabeth Mkwizu alisikiliza maombi hayo jana yanayohusu mshitakiwa kupinga uamuzi uliotolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Geoffrey Mhini juu ya maombi namba 13098/2025 ya upande wa mashitaka kuomba kulindwa kwa mashahidi chini ya kifungu namba 194 cha CPA.

Maombi hayo yaliwasilishwa katika shauri namba 8606/2025 la uchochezi na kuchapisha taarifa za uongo linalomkabili Lissu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu linalosikilizwa mbele ya Hakimu Mhini.

Katika uamuzi huo mahakama iliamuru kuwa mashahidi ambao ni raia wa kawaida kulindwa wakiwa wanatoa ushahidi lakini ambao ni askari watawekwa wazi wakiwa wanatoa ushahidi wao.

Wakipinga uamuzi huo, Mawakili wa mpeleka maombi wakiongozwa na Mpare Mpoki akisaidiana na Dk Rugemeleza Nshala, Jebra Kambole na Jeremiah Mtobesya walidai wana hoja zao nne zinazoungwa mkono na kiapo fungani kuthibitisha ni maombi ya mshitakiwa.

Dk Nshala alidai maombi yaliyotumwa hayakuwa na viapo vya mashahidi ambao walikuwa wanaunga mkono maombi hayo kuthibitisha kweli kuwa mashahidi hao walikuwa wanatishiwa hivyo walihitaji kufichwa au kulindwa kwa usalama wao.

Alidai uamuzi huo ulitolewa kimakosa kwani kiapo cha maandishi kilichoambatanishwa na maombi ni mbadala wa muombaji, pia Wakili Kambole alidai uamuzi uliotolewa haukuwa wa haki kwani uamuzi ulitolewa bila kupima pande zote mbili.

Kambole alidai hakimu alitakiwa kuangalia kuhusu kiapo na kusikiliza upande wa mshitakiwa ndipo atoe uamuzi lakini aliamua bila kuzingatia hilo, pia alidai shauri hilo si la muhimu kiasi hicho hadi kufanya mashahidi wafichwe kama walivyoomba.



Kwa upande wake, Mtobesya alidai kuficha mashahidi ni kuinyima mahakama na mshitakiwa haki yake ya kuangalia mwenendo wa shahidi wakati akitoa ushahidi wake ili kufanya tathmini iwapo anaeleza ukweli au ushahidi wake unatia shaka.

Walidai wanaiomba mahakama ione ulazima wa kupitia maombi yaliyotolewa uamuzi kwa sababu hayajakidhi vigezo kutokana na sababu zao ambazo wameziwasilisha mahakamani hapo.

Akijibu hoja hizo Wakili wa Serikali Mkuu, Nassoro Katuga alidai si kweli kwamba maombi hayo yaliwasilishwa bila kiapo ambatani kwani waliweka viapo viwili vilivyotolewa ambacho kimoja ni cha Tawabu Issa na Mkuu wa Upelelezi Kanda wa Dar es salaam, Faustine Mafwele.

Alidai kupeleka viapo ambavyo vimewataja mashahidi hao hakutokuwa na haja ya kuomba kulindwa kwa mashahidi hao kwani watakuwa wametajwa na mahakama inaendeshwa kwa uwazi, hivyo taarifa za mashahidi zikionekana hakutokuwa na haja ya kuomba kulindwa.

Pia, alidai hakimu kwa utashi wake aliona kuna haja ya mashahidi hao kulindwa na ushahidi huo ulivyokuwa umejitosheleza na busara ikamtuma, hivyo hakukuwa na upendeleo kwani hakuna dosari katika ushahidi huo, pia alidai hawajataja sheria inayoeleza kwamba ukimuona shahidi kwa sura ndio kutakuwa na uamuzi wa haki.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Job Mrema alidai vifungu vilivyopelekwa na wapeleka maombi hao haviwezi kuifanya mahakama ikatoa au ikubali maombi ambayo yamewasilishwa na mpeleka maombi, hivyo aliiomba mahakama itupilie mbali maombi hayo.

Scanned with MOBILE SCANNER

MAHAKAMA

KOSA LA HAKIMU:

# Kesi aliyehukumiwa miaka 30 gerezani kusikilizwa upya

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dodoma imeamuru kesi ya kijana Jafeti Masinga aliyehukumiwa kifungo cha miaka 30 gerezani kwa mashtaka ya kubaka, ianze upya kutokana na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Dodoma kushindwa kuandika sababu za mabadiliko ya mahakimu kwenye mwenendo wa kesi.

Vilevile, mahakama hiyo imeelekeza kesi hiyo isikilizwe kwa haraka na endapo mshtakiwa akipatikana na hatia, muda aliotumikia rumande kabla ya hukumu utapaswa kuzingatiwa na kupunguzwa katika adhabu.

Uamuzi huo wa Rufani ya Masinga ulitolewa na Jaji Suleiman Hassan wa mahakama hiyo wakati rufani ya mshtakiwa yenye hoja 15 ya kupinga adhabu hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kusikiliza. Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Francis Mwakifuna.

Mahakama hiyo baada ya kupitia kwa umakini mwenendo wa kesi ya Mahakama ya Wilaya kwa uamuzi wake binafsi, ilibaini kuwapo dosari za kisheria kuhusiana na utekelezaji kifungu cha 214(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Sura ya 20, Marejeo ya 2022).

Jaji Hassan alisema dosari hiyo inahusiana na mabadiliko ya mahakimu waliokuwa wakisikiliza kesi hiyo bila kufuata taratibu za kisheria. Kabla ya kuendelea kuamua hoja za msingi za rufani hiyo, mahakama iliona ni vyema kuwaalika pande zote mbili kueleza maoni yao.

"Kwa kuzingatia kuwa mrufani ni mtu wa kawaida, asiye na uelewa wa masuala ya sheria na kwa kuwa kasoro iliyobainika ni ya kisheria, mahakama imeona ni busara kwanza kumruhusu Wakili wa Serikali kutoa maoni yake juu ya dosari hii," alisema Jaji Hassan

Kwa kuzingatia hilo, Wakili Mwakifuna alikiri kuwapo dosari hiyo na kudai kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 214(1) cha CPA, pale hakimu aliyekuwa ameshaanza kusikiliza kesi anabadilishwa na hakimu mwingine, ni wajibu wa kisheria kwa hakimu mpya kurekodi sababu za kuchukua uendeshaji kesi hiyo.

Wakili Mwakifuna alidia kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 214(2) cha CPA, Mahakama Kuu ina mamlaka ya kufuta ushahidi uliotolewa baada ya mabadiliko hayo au kuamuru kesi isikilizwe upya.

Kwa upande wa mrufani, hakuwa na hoja ya msingi ya kuwasilisha. Aliacha hatima yake mikononi mwa mahakama.

Jaji Hassan alisema kuwa kwa kuzingatia hoja zilizotolewa na Wakili wa Serikali pamoja na mamlaka za kisheria zinazohusika, suala kuu la kuamua ni ikiwa utaratibu wa kubadilisha hakimu ulicheleweshwa au ulikiukwa.

Alisema kuwa katika kifungu hicho, inaelezwa kwamba hakimu anayechukua nafasi hiyo anaweza kutumia ushahidi au kumbukumbu zilizorekodiwa na mtangulizi wake na endapo akiona inafaa, anaweza kuwaita tena mashahidi na kuanza upya usikilizaji kesi hiyo.

"Kama sheria inavyoelekeza hapo juu, ni lazima kila mara ambapo hakimu anabadilika, sababu za hakimu wa awali kushindwa kumaliza usikilizaji kesi ziwekwe wazi kwa maandishi," alisema Jaji Hassan.

Kwa kuzingatia hayo, Jaji Hassan alisema baada ya kupitia kwa makini mwenendo mzima wa kesi na kuzingatia mazingira ya shauri hilo, ameridhika kuwa kesi hiyo inafaa kusikilizwa upya.

"Ninaamuru kwamba kesi hii isikilizwe upya mbele ya hakimu mwenye mamlaka ambaye hajawahi kuendesha kesi hiyo hapo awali.

"Ninaelekeza zaidi kwamba mahakama hiyo itoe maelezo ya wazi kuhusu sababu za mabadiliko ya hakimu, kwa kuzingatia kifungu cha 214(1) cha CPA," alisema na kuongeza:

"Mahakama ihakikishe mshtakiwa anafahamishwa kuhusu haki yake ya kudai ushahidi usikilizwe upya, kama sheria inavyotaka.

"Mshtakiwa ataendelea kushikiliwa rumande akisubiri usikilizwaji mpya wa kesi. Hata hivyo, suala la dhamana linaweza kufikiriwa upya na kuamuliwa na mahakama," alisema Jaji Hassan.

Jaji huyo pia alielekeza kesi hiyo isikilizwe kwa haraka na endapo mshtakiwa akipatikana na hatia, muda aliotumikia rumande kabla ya hukumu utapaswa kuzingatiwa na kupunguzwa katika adhabu.

Kwa maoni: +255 677 020 701Email: customerrelations@guardian.co.tz



Scanned with

KORTINI

# Mahakama Kuu yaitisha mashauri mawili kufutwa Kanisa la Gwajima

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dodoma imeitisha mashauri mawili yanayohusu kufungwa kwa Glory of Christ Tanzania Church, maarufu Kanisa la Ufufuo na Uzima, linaloongozwa na Askofu Josephat Gwajima.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi nje ya mahakama hiyo, Wakili Peter Kibatala alidai mashauri mawili ni kufutiwa usajili wa kanisa hilo hilo ni pamoja na shauri la kikatiba lililofunguliwa na waumini 52.

"Leo (juzi) tarehe 22 mwezi Julai 2025, mashauri mawili yanayozunguka kufutiwa usajili kwa Glory of Christ Tanzania Church, maarufu Kanisa la Ufufuo na Uzima, linaloongozwa na Askofu Josephat Gwajima,yaliitwa mahakamani.

"Shauri la kwanza ni namba 16408 la mwaka 2025, ambalo lilifunguliwa na waumini 52 wakiongozwa na Dinal Mbaga na wenzake 51, linalosikilizwa mbele ya jopo la majaji watatu wakiongozwa na Jaji wa Mahakama ya Rufani Cyprian Mkeha," alidai.

Wakili huyo alidai jopo hilo linasikiliza shauri la kikatiba ambalo liliitwa kwa njia ya mtandao kutokana na sababu za kimahakama.

"Kwa kawaida mashauri huendeshwa kwa njia ya mbili; njia namba moja ni ya kimtandao na njia ya pili ni kufika mahakamani.

"Shauri la kwanza la kikatiba ambalo wadaiwa ni Dinal Mbaga na wenzake 51 wanalalamikia taasisi mbili. Taasisi ya kwanza ni Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania, siyo kama mtu bali ni kama taasisi. Jeshi la Polisi linatenda kazi zake, matendo yake yote chini ya mwamvuli wa kisheria wa kiutendaji chini ya mwamvuli wa IGP," alidai.

Wakili huyo alidai kuwa IGP ni mdaiwa wa kwanza na mdaiwa wa pili ni Ofisi ya



**Shauri la kwanza la kikatiba ambalo wadaiwa ni Dinal Mbaga na wenzake 51 wanalalamikia taasisi mbili. Taasisi ya kwanza ni Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania, siyo kama mtu bali ni kama taasisi. Jeshi la Polisi linatenda kazi zake, matendo yake yote chini ya mwamvuli wa kisheria wa kiutendaji chini ya mwamvuli wa IGP.**

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo Dinali Mbaga na wenzake 51 katika shauri hilo wana hoja kwamba Jeshi la Polisi limekuwa linakiuka haki za kikatiba.

"Kuna haki mbili za kikatiba, kuna haki za kuabudu na haki ya kufurahia uhuru ambazo zipo katika Ibara ya 15 na 19, wanalalamika utendaji wa Jeshi la Polisi ambao umekiuka haki hizo kwa kuwa umewakamata na umewanyanyasa kisheria, haukuwafikisha katika vyombo vyovyote maalum vya kisheria ambavyo vinahusika na kutoa adhabu kwa watu ambao wamevunja sheria na umeingilia kabisa uhuru wao wa kuabudu na kuwasiliana na Mungu wao," alidai.

Wakili Kibatala alidai shauri hilo liliitwa juzi na wamepanga ratiba na wenzao wa upande wa se[illegible] ambao wana mapinga[illegible] ya kisheria, wakidai k[illegible] ba Dinal Mbaga na wenzake wana tiba mbadala.

"Yaani wanaweza kupata nafuu zingine za kisheria kwa utaratibu mwingine kwa hiyo tutajadili hayo kisheria na mahakama itatoa uamuzi Agosti 29, 2025 na hivi sasa imetoa ratiba ya kubadilishana hoja kimaandishi.

"Jambo la msingi ni uamuzi kuhusu mapingamizi hayo ya serikali, ambao utatolewa tarehe 29 mwezi Agosti. Hilo ndilo shauri la kwanza ambalo lilifanyika asubuhi leo (juzi)," alidai.

Wakili Kibatala alidai shauri la pili ni lililofunguliwa na Glory of Christ Tanzania Church kupinga utaratibu uliotumika kulifutia kanisa hilo usajili.

"Sasa kanisa limechukua hatua hiyo baada ya kupata waraka ambao unasemekana ni wa kulifutia usajili kanisa hilo. Tumekata rufani Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Wakati tunasubiri rufani ifanyiwe kazi na michakato yote, tumekuja mahakamani kuomba ipatikane zuio la muda mpaka waziri atakapomaliza michakato yake.

"Wakati michakato ya waziri inaendelea, basi haki zao kama kanisa zisisumbuliwe mpaka uamuzi wa waziri ufanyiwe kazi na kuamuliwa kwa mujibu wa sheria.

"Hivyo, leo (juzi) tumefika mbele ya Jaji Masabo na tumepangiwa ratiba ya kuleta kiapo kinzani na wenzetu wataleta kiapo kinzani na tutakutana hapa tarehe 12 mwezi Agosti mwaka huu kwa ajili ya usikilizwaji shauri hili," alidai.

Wakili Kibatala alidai Kanisa la Ufufuo na Uzima litaendelea hadi alichoita "tone la mwisho" kufuatilia haki zake za kufanya shughuli za ibada kwa niaba yake na waumi wake.

***Kwa maoni: +255 677 [illegible], email: customerrelations@[illegible]***



KORTINI

# Lissu aipa angalizo Mahakama Kuu

**Na Grace Gurisha**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ameipa angalizo Mahakama Kuu Masjala Ndogo ya Dar es Salaam isije ikaruhusu kuwa Mahakama ya Kijeshi baada ya Askari Magereza kutaka kukagua nyaraka alizopewa na wakili wake kama ni salama au la.

Lissu amedai kwamba nyaraka zake haziwezi kushikwa na Askari hao kwa sababu sheria haimtaki kufanya hivyo kwa kuwa inaruhusu wakili kuzungumza na mteja wake ndani ya chumba cha mahakama.

Alidai hayo jana mbele ya Jaji Elizabeth Mkwizu wa mahakama hiyo kabla ya usikilizwaji maombi ya marejeo ya uamuzi wa kukubali kuficha mashahidi katika kesi ya kuchapisha taarifa za uongo mtandaoni yalitolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Baada ya pande zote mbili kueleza mahakama kuwa ziko tayari kwa usikilizwaji maombi hayo, Wakili wa Lissu, Mpale Mpoki, alidai kuwa kuna masuala ambayo walihitaji mahakama iyaweke sawa kuhusu mshtakiwa kuzungumza na mawakili wake.

"Tunataka Mahakama itupe mwongoza kwa sababu tunapata ugumu sana kuwasiliana na mteja wetu. Ni haki ya mleta maombi kuzungumza na wakili wake akiwa mahakamani. Asubuhi tulitaka kuzungumza naye kuhusu kitakachofuata kuhusu haya maombi ikashindikana.

"Kwa sababu tumeambiwa na Askari Magereza licha ya kwamba sisi ni maofisa wa mahakama lakini kunakuwepo na mipaka," alidai Wakili Mpoki.

Baada ya Jaji Mkwizu kumwuliza swali Wakili Mpoki, aliamua kumwachia Lissu kuieleza mahakama ambacho kimetokea na alipewa nafasi na kuanza kuzungumza.

"Tatizo hili si la leo (jana) tu. Limeanza siku ya Ijumaa kwenye uamuzi hapa. Mheshimiwa Jaji nilipofika mahakamani kabla hata mahakama haijafunguliwa hata makarani hakuna, nikapelekwa lokapu (rumande) hadi pale kesi ilipoitwa saa 6:00 mchana. Katika kipindi chote niliwaomba askari waniitie wakili wangu ili tushauriane lakini hakuja," alidai Lissu.



**Siku hiyo ya Ijumaa, Wakili Nashon Nkungu aliniletea nyaraka hapa kizimbani, askari wakazinyakua wakazipeleka huko chini. Nilipoanza kuzidai wakasema huwezi kuzipata wakazirudisha.**

**Tundu Lissu**

Alidai kwamba alimwuliza Wakili Dk. Rugemeleza Nshalla kwa nini hawakuja mahabusu, akadai kwamba aliwaomba askari lakini walimkatalia. Hadi jaji anaingia mahakamani hawakupata muda wa kushauriana na mawakili wake na kukabidhiana nyaraka.

"Siku hiyo ya Ijumaa, Wakili Nashon Nkungu aliniletea nyaraka hapa kizimbani, askari wakazinyakua wakazipeleka huko chini. Nilipoanza kuzidai wakasema huwezi kuzipata wakazirudisha," alidai Lissu.

Aliendelea kudai kwamba jana waliitwa mapema mahakamani, Wakili Paul Kisabo alimpelekea nyaraka kizimbani zinazohusiana na mashauri hayo, akataka kumkabidhi akazuiwa.

"Wakadai kwamba 'ni marufuku mawakili kukupa nyaraka'. Sasa ninashangaa Askari Magereza ndiyo wanaamua ndani ya chumba cha mahakama? Hii si mahakama ya kijeshi, bali ni Mahakama Kuu ya Tanzania.

"Lakini kwa kuangalia hii mahakama imegeuka kuwa ya kijeshi, ona walivyovaa. Mheshimiwa Jaji ukiwa mahakamani, mahakama ni yako. Wewe ndiye bosi, hakuna askari Magereza wala askari polisi," alidai Lissu.

"Hawatakiwi kushika nyaraka zozote. Sasa Mheshimiwa Jaji wewe ndiye utuambie wana haki ya kushika nyaraka zangu? Rai yangu mahakama yako tukufu isije ikaruhusu kuwa mahakama ya kijeshi. Naomba utoe uamuzi uthibitishe kwamba sitakiwi kubuguziwa na hawa mabwana jela, wewe wanaweza kukusikia," aliongeza.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa Serikali Mkuu, Nassoro Katuga, alidia kuwa Jeshi la Magereza limepewa mamlaka ya kuwahifadhi wafungwa na ambao si wafungwa wanapokuwa mahabusu.

Wakili Katuga alidai kuwa katika majukumu hayo, Magereza imepewa sheria ya kuwalinda wafungwa na mahabusu wengine. Alidai Sheria ya Magereza Kifungu 77(I) imezungumizia vitu vingi ambavyo havitakiwi kufanywa kwa ajili ya usalama wao na magereza kwa ujumla.

Pia alidai kuwa sheria hiyo haimruhusu Askari Magereza kuingiza nyaraka yoyote hapo atakuwa ametenda kosa kwenye kazi zao na kwamba hayo yamewekwa kwa ajili ya usalama wa Magereza na kwa mshtakiwa mwenyewe.

Pia alidai kuwa Askari Magereza anaruhusiwa kukagua kujua ni kitu gani hicho ili ajiridhishe kama kina madhara au la.

"Sisi tunaona Magereza haijakosea. Wanatakiwa kufuta utaratibu. Hiki kitu hakijazuiwa wanatakiwa wafuate utaratibu wa kisheria ambazo tumezitunga wenyewe," alidai.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote, Jaji Mkwizu alisema atatoa uamuzi huo kwa pamoja na ule wa maombi ya marejeo yaliyowasilishwa na Lissu kupinga uamuzi wa kuficha mashahidi katika kesi inayomkabili ya kuchapisha taarifa za uongo mtandaoni.

Ilidaiwa kuwa Aprili 3, 2025 jijini Dar es Salaam mshtakiwa Lissu akiwa na lengo la kulaghai umma alichapisha taarifa hizo kupitia mtandao wa YouTube ambapo maneno hayo yalisomeka: 'Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka jana, wagombea wa CHADEMA walienguliwa kwa melekezo ya Rais'.



miradi mbalimbali ya maendeleo nchini. (Picha na Venance Nestory).

# Toleo la sheria zilizotafsiriwa Kiswahili kutoka mwezi ujao

MWANDISHI Mkuu wa Sheria, Onorius Njole amesema toleo la sheria ambazo zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili zitaanza kutoka Agosti mwaka huu.

Njole ameeleza hayo jana katika Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara 'Sabasaba' yanayoendelea mkoani Dar es Salaam.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliagizwa kutafsiriwa kwa sheria ili kueleweka kwa urahisi na watu wa makundi yote.

"Pamoja na hatua kubwa iliyofanyika ya urekebu aliagiza pia kukamilisha kutafsiri sheria," alisema.

Njole alisema sambamba na kuendelea na mchakato wa kukamilisha hilo, pia ofisi hiyo imefanya mabadiliko makubwa ya kuhakikisha sheria zilizopo zinatekelezeka na kuwafikia wananchi.

"Tumefanya mabadiliko makubwa ya kuhakikisha tunakuwa na sheria zinazowafikia wananchi kama sheria na ukamilifu wake na lugha ambayo wananchi wanaifahamu," alisema.

Alisema ofisi hiyo imefanyiwa urekebu wa sheria mbalimbali ili ziweze kuendana na mahitaji ya sasa ya nchi.

"Tumefanya urekebu wa sheria hizi kwa kuzikusanya sheria zote za nchi pamoja na kuingiza marekebisho ambayo yamekuwa yakifanyika kila wakati," alisema.

Aidha, alisema serikali ipo katika mchakato wa kutengeneza mfumo wa sheria wa kusimamia matumizi ya Akili Mnemba (IA) na kubainisha kuwa mchakato huo utakapokuwa tayari utaandaliwa sheria.

"Mfumo mahususi kwa ajili ya AI unafanyiwa kazi na serikali, utakapokuwa tayari utaandaliwa muswada wake na mwisho wa siku itakuja kuwa sheria ni mambo ambayo serikali imeyaona na itayawekea utaratibu wa kisheria," alisema.

Kwa upande wake, Mwandishi Mkuu Msaidizi wa Sheria, Rahema Katuga alisema baada ya kukamilika kwa urekebu wa sheria mbalimbali ambazo zimeanza kutumika Julai Mosi mwaka huu, za awali hazitatumika tena.

"Mahakamani au sehemu yoyote mtu akitaja vifungu vya sheria atatakiwa kutaja hivi ambavyo vimeanza kutumika Julai Mosi," alisema.

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Kheri James, akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi katika siku ya pili ya ziara yake ya kikazi. (Picha na Esta Malibiche).

kesi itakapotajwa tena.

# Jaji Salma asisitiza uandishi wa kesi wenye kuzingatia matakwa kisheria

JAJI Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam, Salma Maghimbi, amesema kuwepo kwa mafunzo ya uandishi wa kesi utasaidia uandishi wa hukumu unaokidhi matakwa ya kisheria na kueleweka katika jamii.

Maghimbi, aliyasema hayo wakati akizungumza katika mafunzo ya Uandishi wa Hukumu kwa Wanasheria, Mamawakili, Makadhi, Mahakimu na Wanafunzi wa chuo cha Sheria ambapo mafunzo yamefanyika katika Mahakama kuu ya

Zanzibar Tunguu Wilaya ya Kati Unguja.

Alisema, uandishi wa hukumu unatakiwa kuzingatia misingi kabla ya kuandika hukumu hizo na jinsi ya kuandika hukumu kwa mujibu wa Sheria na mambo yanayozingatiwa na kutokufanya kabla ya kuandika hukumu.

Pia, alisema endapo mshitakiwa akiwa hajaridhishwa kutokana na alipopelekwa mahakamani anaweza kuomba marejeo na mapitio ama kukata rufaa.

Jaji huyo alisisitiza kuwa uandishi huo wa hukumu hutoa maamuzi kwa kutumia sababu ambazo zilizompelekea kutoa hukumu sambamba na kutumia sheria inayohusika na kesi yenyewe.

Naye, Naibu Mrajis wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Khamis Rashid Khamis, alisema hukumu ni kiini cha maamuzi ya mahakama ambapo kazi ya mwisho wa mahakama ni kutoa hukumu.

Alisema, uandishi wa hukumu unaweza kufanywa kwa lugha zote mbili ikiwemo ya kiswahili na kingereza ambapo ni matakwa ya Sheria kwa hakimu anayehusika katika uandishi wa hukumu yake kutaka kuandika na kulingana na wadau waliokuwepo mbele yake.

Pia, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwani yanakuza ueledi, uwezo na maarifa ya mtendaji katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

"Hukumu inatafsiri haki za watu ambapo inatoa furaha na kuchochea jamii na kujenga amani kwani hukumu inaleta furaha kwa haki za watu," alisema.

Alisema kila hakimu ana weledi na tafsiri ya sheria na hakuna hakimu au jaji anayepotezea haki za watu na kwamba endapo mtu akiwa hajaridhishwa na hukumu iliyotolewa imewekwa rufaa ili kuona haki ya mtu inaendelea kutolewa kwa mujibu wa Sheria na mtu anavyoona inafaa.

Mapema, Naibu Mkuu wa chuo cha Sheria Zanzibar anayesimamia taaluma, Msemo Mavare, alisema matarajio ya chuo hicho cha sheria ni kuona hukumu zinazotolewa zimekidhi vigezo kwa mujibu wa sheria.

Scanned with MOBILE SCANNER

**OMBI>> Mshitakiwa anamwomba DPP kuingia makubaliano ya kumaliza kesi**

# Mazungumzo kati ya DPP, Kurwa Mathias kuendelea

**Na SYLVIA SEBASTIAN**

OFISI ya Mkurugenzi wa Mashitaka nchini (DPP) inatarajiwa leo kuendelea na mazungumzo na mshitakiwa Kurwa Mathias anayedaiwa kusafirisha dawa za kulevya aina ya bangi.

Hatua hiyo inatokana na Mathias kuandika barua kwenda ofisi ya DPP kuomba kuingia makubaliano ya kumaliza shauri hilo.

Wakili wa Serikali, Tumaini Mafuru alidai hayo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wiki iliyopita, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Rahim Mushi, shauri lilipopelekwa kwa kutajwa.

"Mshitakiwa Mathias aliomba kuzungumza na ofisi ya DPP, hivyo barua yake imepokelewa tutaendelea na mazungumzo ya kumaliza shauri hilo," alidai Wakili Mafuru.

Mathias na Edina Paulo wanakabiliwa na shtaka la kusafirisha dawa za kulevya.

Kwa mujibu wa hati ya mashitaka, Mathias ambaye ni mkazi wa Salawe, Shinyanga na Edina wa Tabora, Urambo, wanadaiwa kutenda kosa, Mei 11, mwaka jana, eneo la ukaguzi wa mizigo Bandari ya Dar es Salaam.

Inadaiwa washitakiwa walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya bangi zenye uzito wa gramu, 512,50.

Hakimu Mushi aliahirisha shauri hilo hadi leo kwa kutajwa na washitakiwa wapo mahabusu.

**MAFUNZO**



MAJAJI, watendaji na aadau wa Mahakama, wakisikiliza hotuba ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi, Dk. Yose Mlyambina (hayupo pichani) katika i mafunzo yaliyotolewa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), jijini Mwanza, juzi. (Na Mpigapicha Wetu).

# Atuhumiwa kuiba simu Coco Beach

**Na HAWA NGADALA**

MKAZI wa Gombolamboto, Dar es Salaam, Hilal Shirima amefikishwa Mahakama ya Mwanzo Kinondoni, akikabiliwa na shtaka la wizi wa simu yenye thamani ya sh. 900,000.

Shirima (32) alifikishwa mahakamani hapo, wiki iliyopita na kusomewa shtaka na Mwendesha Mashitaka, Yona Stayoni, mbele ya Hakimu Mfawidhi, Olivia Towilo.

Stayoni alidai mshitakiwa alitenda kosa, Juni 26, mwaka huu, maeneo ya Coco Beach, wilayani Kinondoni.

Inadaiwa mshitakiwa aliiba simu aina ya REDMI BLUE MAX yenye thamani ya sh. 900,000, mali ya Ally Said.

Mshitakiwa alikana kutenda kosa, upande wa mlalamikaji ulidai una mashahidi waliokuwepo siku ya tukio.

Hakimu Olivia alimweleza mshitakiwa shtaka linalomkabili linadhaminika kwa mujibu wa sheria na kumtaka awe na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho kutoka ofisi za kata na vitambulisho vya Taifa.

Aidha, wadhamini walitakiwa kila mmoja kutia saini fungu la dhamana la sh. 500,000.

Pia, aliutaka upande wa mlalamikaji kufika tarehe itakayopangwa na mashahidi kwa usikilizwaji.

Mshitakiwa alirudishwa mahabusu, baada ya kushindwa kutimiza masharti na shauri liliahirishwa hadi Agosti 7, mwaka huu.

**Masharti**

**DHAMANA**

Mshitakiwa alitakiwa awe [illegible] wawili wenye barua za utar[illegible] [illegible]toka ofisi za kata na vitambulish[illegible]

# Kesi uhujumu uchumi kuendelea Julai 25

**Na SYLVIA SEBASTIAN**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imepanga Julai 25, mwaka huu, kuendelea na usikilizwaji wa kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Hassan Shabani na wenzake.

Shabani na wenzake wanadaiwa Agosti 28, 2019, walikutwa na nyara za serikali zenye thamani ya zaidi ya sh. bilioni 4.4.

Hakimu Mkazi Mkuu, Aaron Lyamuya, alipanga tarehe hiyo, wiki iliyopita baada ya upande wa jamhuri kudai shahidi waliyekuwa wanamtegemea kutoa ushahidi amepata dharula ya kifamilia.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Monica Ndakidemi akishirikiana na Wakili wa Serikali, Tumaini Mafuru, waliomba radhi kwa kuwa hawajamwandaa shahidi mwingine wa kuendelea na usikilizwaji wa kesi.

"Upande wa jamhuri tulimwandaa shahidi ambaye ushahidi wake ni mrefu, lakini kwa bahati mbaya amepata dharula ya kifamilia, tunaomba radhi," waliomba mawakili hao.

> **"Upande wa jamhuri tulimwandaa shahidi ambaye ushahidi wake ni mrefu, lakini kwa bahati mbaya amepata dharula ya kifamilia, tunaomba radhi...**
>
> Upande wa jamhuri

Kwa upande wa Wakili wa utetezi, Nehemiah Nkoko, alidai kwa kuwa upande wa jamhuri umeomba radhi, hakuna budi kuahirisha shauri hilo na kupanga tarehe ya karibu.

Shabani, Olivia Mchuwa, Haidary Sharifu, Joyce Thomas, Abdul Hamisi na Salama Mshamu wanakabiliwa na mashitaka ya kujihusisha na vipande 413 vya meno ya tembo na viwili vya meno ya kiboko.

Washitakiwa wanadaiwa kujihusisha na nyara hizo za serikali bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Pia, washitakiwa wanadaiwa kuongoza genge la uhalifu kwa kukusanya, kununua, kuuza na kusafirisha nyara za serikali.

Hakimu Lyamuya aliahirisha kesi hadi Julai 25, mwaka huu, kwa kuendelea na usikilizwaji wa mashahidi wa upande wa jamhuri.

Scanned with MOBILE SCANNER

## HABARI KITAIFA

UWAJIBIKAJI

# THBUB yataka Sheria ya Uvuvi ifumuliwe

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Mohamed Khamis Hamad, ameshauri kada ya sheria kuimarisha mifumo ya sheria ikiwamo kubadilisha baadhi ya sheria zake ili kulinda haki za watu.

Mohamed alisema hayo wakati wa mkutano maalum ulioweka pamoja THBUB na wadau wengine wa sekta ya uvuvi uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi.

Alieleza kuwa kufanyiwa marekebisho kwa sheria hizo, hasa Sheria ya Uvuvi kutasaidia kulinda haki za wavuvi wadogo katika kulinda na kutetea ustawi wao.

Akizungumzia changamoto zinazowakabili wavuvi hao, Mohamed alieleza kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kutatuliwa kisheria hasa kujengea uelewa jamii ya wavuvi wadogo pamoja na kuongeza uelewa wa haki za binadamu kwa jamii.

Mohamed pia alishauri serikali kuwashirikisha wavuvi wadogo hasa wakati wa kupanga mikakati inayolenga kulinda rasilimali za bahari ili kutokiuka haki za binadamu.

Katika mkutano huo, kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Agness Meena, Mkurugenzi wa Uvuvi Tanzania, Prof. Mohamed Sheikh alibainisha haki za wavuvi wadogo ni msingi wa maendeleo endelevu kwenye sekta ya uvuvi nchini.

"Wavuvi wadogo ni muhimili mkubwa katika uchumi wa jamii za pwani na usalama wa chakula nchini. Ni wajibu wetu kuhakikisha wanashirikishwa kikamilifu katika usimamizi wa rasilimali za bahari, wanalindwa dhidi ya unyanyasaji wa mifumo ya kisheria, na wanapewa elimu ya kutosha kuhusu matumizi endelevu ya bahari," alieleza.

Prof. Mohamed alisisitiza haki huenda sambamba na wajibu, hivyo zinapoelezewa haki za wavuvi ni vyema pia kukaelezwa na wajibu wa wavuvi.

Mkutano huo uliandaliwa na tume hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Denmark ya Haki za Binadamu kwa lengo la kukuza uelewa wa pamoja juu ya haki za binadamu zinavyohusiana na upatikanaji na usimamizi wa pamoja wa rasilimali za bahari kwa wavuvi wadogo, kuunda muhtasari wa pamoja wa mijadala ya kitaifa na kubaini mbinu bora na suluhisho za changamoto zinazowakabili wavuvi wadogo.

Pia ulijadili haki za wavuvi wadogo katika upatikanaji na usimamizi wa pamoja wa rasilimali za bahari pamoja na kuwaweka pamoja wawakilishi kutoka serikalini, asasi za kiraia, vyama vya wavuvi, wataalam wa mazingira ya bahari na mashirika ya kimataifa yanayoshughulika na maendeleo ya sekta ya uvuvi.



Abubakari Msangi (48) akiwa chini ya ulinzi wa Askari wa Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 20 jela kwa kosa la kukutwa na vipande saba vya meno ya Tembo na Kiboko vyenye thamani ya sh. milioni 41. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

MAHAKAMANI

# Mshtakiwa kesi dawa za kulevya aachiwa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi, imemwachia huru mshtakiwa Ally Sefu baada ya kumwona hana kesi ya kujibu katika shtaka la kusafirisha viroba 11 vya dawa za kulevya aina ya bangi.

Uamuzi huo wa mahakama ulitolewa jana mbele ya Jaji Sedikia Kisanya baada ya Jamhuri kufunga kesi kwa upande wao.

Washtakiwa katika shauri hilo walikuwa wawili, Peter Mdegela na Sefu. Wote walidaiwa kuwa Septemba 7, 2017, katika mtaa wa Tarangire Mbezi Beach, walikutwa na viroba 11 vya bangi.

Akiwasilisha hoja mahakamani, Wakili wa Serikali Marietha Maguta alidai upande wa Jamhuri unafunga kesi. Mashahidi waliowaleta wanatosha.

Baada ya kudai hayo, mawakili wa upande wa utetezi Yohana Kibindu na Charles Fredrick hawakuwa na pingamizi.

Akitoa uamuzi Jaji Kisanya alisema upande wa Jamhuri katika shauri hilo uliita mashahidi watano na vielelezo sita katika kuthibitisha mashtaka.

"Baada ya Jamhuri kufunga ushahidi, mahakama inaangalia kesi ya msingi kama ipo ili washtakiwa wajitetee.

"Upande wa Jamhuri una wajibu wa kuonesha kuwapo kesi ya msingi. Baada ya kupitia, ushahidi unaunga kesi ya msingi dhidi ya mshtakiwa wa kwanza pekee, Peter.

"Ushahidi unaonesha viroba 11 vya bangi vilichukuliwa kwa mshtakiwa wa kwanza na uchunguzi ulithibitisha ni dawa za kulevya aina ya bangi," alisema Jaji Kisanya.

Alisema mshtakiwa wa pili, Sefu upande wa mashtaka haukuleta ushahidi kuonesha kama mshtakiwa huyo alisafirisha dawa za kulevya.

Alisema mshtakiwa wa pili alihusishwa kwenye shauri kutokana na maelezo ya mshtakiwa wa kwanza.

"Mahakama inaona kuna kesi ya msingi dhidi ya mshtakiwa Peter, anatakiwa ajitetee. Mahakama inamwachia huru mshtakiwa wa pili, Ally Sefu baada ya kumwona hana kesi ya kujibu," alisema Jaji Kisanya.

Wakili Yohana alidai mshtakiwa Peter atajitetea kwa kiapo na hatakuwa na shahidi wala kielelezo cha kuwasilisha.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**




Scanned with MOBILE SCANNER





MALIASILI

# Waziri awa mbogo uvunjaji sheria kipindi cha uchaguzi

Na Paul Mabeja, DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amesema mtu yeyote atakayevunja sheria katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu achukuliwe hatua bila kujali nafasi yake bila ili iwe fundisho kwa wengine.

Ndumbaro, alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa, wakati wa hafla ya kukabidhi magari 16 kwa ajili ya ofisi za taifa za mashtaka za wilaya nchini.

Alifafanua kuwa ametoa kauli hiyo kutokana na uzoefu kuonesha wakati wa kipindi hicho watu wengi wamekuwa wakivunja sheria.

Alisema Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS), inapaswa kuongeza umakini katika utekelezaji wa majukumu yake ili kukabiliana na hali hiyo.

Alisema kipindi hicho watu wengi wamekuwa wakifanya mambo mengi ya uvunjifu wa sheria za nchi wakihisi zinakuwa zimekwenda likizo.

"Wakati wa Uchaguzi Mkuu uzoefu unaonesha kuwa watu wamekuwa wakifanya mambo ambayo yanatishia uvunjifu wa amani wakihisi kuwa sheria zipo likizo.

**"Wakati wa Uchaguzi Mkuu uzoefu unaonesha kuwa watu wamekuwa wakifanya mambo ambayo yanatishia uvunjifu wa amani wakihisi kuwa sheria zipo likizo.**

"Naomba niwaambie kuwa wakati wa uchaguzi mkuu sheria haziendi likizo zinakuwepo, hivyo ofisi ya taifa ya mashtaka mnapaswa kuongeza umakini kipindi hiki na kwa yeyote ambaye atabainika kuvunja sheria achukuliwe hatua bila kujali nafasi yake," alisema Ndumbaro.

Alionya kuwa kama watu hao hawatachukuliwa hatua wanaweza kuwa chanzo cha uvunjivu wa amani iliyodumu kwa muda mrefu nchini, hivyo NPS wanapaswa kuwachukulia hatua mara watakapo wabaini.

"Kama mgombea ataachwa atumie jukwaa la kampeni kutukana wengine na wengine nao wakatumia jukwaa hilo kujibu matusi hayo halafu wakaachwa tu watafikiri kuwa sheria zipo likizo, lakini kama watakamatwa itakuwa fundisho kwa wengine," alisema.

Kuhusu kampeni ya msaada wa sheria ya Mama Samia, alisema imewasaidia kubaini kukithiri kwa matukio ya ukatilii wa kijinsia, migogoro ya ardhi na mirathi.

"Kampeni hii imetusaidia kubaini ongezeko la ukatilii wa kijinsia, wapo wanawake na watoto wanafanyiwa vitendo vya ukatilii nchini, ofisi hii lazima muone ni namna gani inaweza kushughulikia suala hili," alisema.

Scanned with Mobile Scanner



# Legal aid mediation end 18-year land feud

By AHMADA YAHAYA

A LONG-STANDING land dispute between two residents of Mbezi Msumi in Ubungo District, Dar es Salaam Region Adelina Nyaulingo and Josephine Mshana has finally been resolved, thanks to the ongoing Mama Samia Legal Aid Campaign currently active at the 49th Dar es Salaam International Trade Fair (DITF).

The conflict, which had persisted for over 18 years, came to a peaceful resolution through voluntary mediation facilitated by legal experts from the Mama Samia Legal Aid Campaign.

As part of the agreement, Ms Nyaulingo consented to vacate the contested land, while Ms Mshana agreed to construct a new two-room house for her on an alternative plot within the same area.

Speaking to the media, Mr Marco Petro, a Legal Officer from the Ministry of Constitution and Legal Affairs, explained that the dispute began in 2007, when Ms Nyaulingo purchased the land from a seller who was later found not to be the rightful owner.

"Ms Nyaulingo believed she had legally acquired the land and even began developing it," said Mr Petro. "However, in 2008, a resident named Yasin Mpogoro came forward and proved that he held the legal title to the land."

Following a court ruling in his favour, Mr Mpogoro legally sold the land to Ms Mshana, rendering Ms Nyaulingo an illegal occupant, albeit unknowingly.

Mr Petro noted that for years, Ms Mshana attempted various legal and administrative avenues to reclaim her land. However, efforts were stalled due to Ms Nyaulingo's difficult living conditions and the potential for social unrest, as both parties stood firmly on their positions.

The turning point came when legal campaign intervened. Legal officers reviewed all documents, consulted local leaders and land officers and engaged both parties directly. After thorough verification, including court judgments and title deeds, it was confirmed that Ms Mshana was the rightful landowner.

"In a spirit of compassion, Ms Mshana agreed to provide Ms Nyaulingo with a new home, a two-room house on a separate plot secured with the help of her family.

Construction will begin immediately and once complete, Ms Nyaulingo will relocate, allowing Ms Mshana to fully occupy her land," Mr Petro said.

He added that this successful mediation highlights the importance of alternative dispute resolution in fostering justice, peace and social harmony.

Ms Nyaulingo expressed gratitude for the peaceful outcome. "Thanks to MSLAC's mediation, I've been relocated to a new plot and Ms Mshana has agreed to build me a two-room house. I am truly thankful," she said, urging others with legal challenges to seek assistance through the campaign.

Ms Mshana also thanked Ms Nyaulingo for agreeing to the settlement and praised the mediation efforts.

"I deeply appreciate Ms Nyaulingo's wisdom and willingness to resolve this peacefully. This is a victory for justice and unity. After many years of struggle, we've found a fair and compassionate solution," she said.

Powerful boost

Planning Ministry backs

SHERIA

# Maombi kupinga kanuni za maadili uchaguzi yatupwa

Daniel Mjema, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Dodoma.** Mahakama Kuu ya Tanzania imetupilia mbali maombi ya Watanzania wawili, Kumbusho Kagine na Bubelwa Kaiza, waliokuwa wakiomba kibali cha kufungua maombi ya mapitio ya mahakama kupinga Kanuni za Maadili ya Uchaguzi Mkuu 2025.

Walifungua maombi namba 12670 ya mwaka 2025 dhidi ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), wakiomba waruhusiwe kufungua maombi kupinga matumizi ya kanuni hizo.

Kanuni hizo zimesainiwa na vyama 18 vya siasa nchini, isipokuwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), ambacho kinashinikiza mabadiliko ya mifumo na sheria ya uchaguzi, zikiwamo kanuni hizo.

Uamuzi huo ulitolewa Julai 11, 2025 na Jaji Abdi Kagomba wa Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dodoma na kupatikana mtandaoni Julai 15, 2025.

Jaji Kagomba ameeleza kuwa kifungu namba 162 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2024, ambacho ndicho kilichotumika kutengeneza kanuni hizo, kinaonyesha kuwa waombaji si wadau wa kanuni hizo.

Kifungu kidogo (1) kinasema: "Kwa madhumuni ya kusimamia uchaguzi wa haki, huru na amani, na baada ya kushauriana na vyama vyote vya siasa na serikali, tume itaandaa na kuchapisha katika Gazeti la Serikali, kanuni hizo za maadili."

Kanuni hizo ndizo zitakazoainisha maadili ya vyama vya siasa, Serikali na INEC wakati wa kampeni za uchaguzi, uchaguzi wenyewe, pamoja na utaratibu na utekelezaji wake.

Kifungu kidogo (2) kinasema kanuni za maadili ya uchaguzi zitasimamiwa na kila chama cha siasa, kila mgombea kabla hajawasilisha fomu ya uteuzi, serikali na tume, na zitapaswa kuzingatiwa na wahusika wote waliosaini kanuni hizo.

Jaji amesema kanuni hizo zinaeleza madhumuni ya kusimamia maadili na nani watashirikishwa kabla hazijatangazwa; na imetaja pia ni nani watazisaini, ambao ni vyama, INEC, serikali na wagombea.

"Inaonekana wazi kwangu kwamba hii ni sheria maalumu kwa kundi maalumu la wadau, kama vile ambavyo uamuzi wa mahakama huwa unawabana pande zile tu ambazo zilihusika na shauri hilo," alisema.

"Swali linaweza kuwa, ni kwa vipi kifungu 162 kinahusiana na masilahi ya kutosha ya waleta maombi katika shauri hili. Kama alivyoeleza Wakili wa Serikali, ni lazima mwombaji aoneshe masilahi katika mapitio hayo ya mahakama anayoyaomba," alisema na kuongeza:

"Sioni sababu zenye mashiko za kuishawishi mahakama hii ni kwa vipi (waombaji) ni washirika. Mtu anaweza kujiuliza, wako wapi wadau waliochukizwa ambao, bila kuwa na mashaka, Mahakama inaweza kuwatambua."

Amesema: "Bila wao kuwapo mbele ya Mahakama hii, hiki kilichosemwa na waombaji katika sababu ya 6.1, 6.2, 6.3, 6.4 na 6.5 ya maelezo yao kinakuwa batili, kutokana na ukweli kuwa wao ni majirani tu na si wenye haki ya kushtaki."

"Hata katika sababu ile ya 7.0 kwamba waombaji wana masilahi na uchaguzi wa huru na haki, inaweza tu kuonekana kama masilahi ya mbali na si masilahi ya kutosha katika masuala yaliyoibuliwa na waombaji," alisema.

"Ni kutokana na sababu hizo, na ukweli kuwa kuna tofauti ya majina kama yanavyoonyeshwa kwenye kiapo chao na yale yanayoonekana katika vitambulisho vya kupigia kura, na hakuna kiapo kinachoonyesha kuwa majina hayo hutumika kwa pamoja, ninaona kabisa wameshindwa kuishawishi Mahakama juu ya masilahi yao," alisema na kuongeza:

"Hivyo, kutokana na uchambuzi huo, maombi ya kuzuia matumizi ya kanuni hizo yanakosa miguu ya kusimamia, na kwa sababu kanuni hizo ni kwa ajili ya wadau mahususi na waombaji hawamo, basi maombi yao yanatupiliwa mbali."

### Hoja za waleta maombi

Wakiomba kupatiwa kibali cha kufungua maombi ya kupinga kanuni hizo, waombaji walieleza kuwa Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za mwaka 2025 zilichapwa katika gazeti la Serikali la Aprili 18, 2025. Wanazipinga wakidai zinakiuka utaratibu kwa kiasi kikubwa, hazina maana wala mantiki, zina makosa ya sheria kwenye kumbukumbu, na zinakiuka sheria na kanuni nyinginezo, pamoja na kutangazwa bila mashauriano.

Kupitia maombi hayo, kama wangepatiwa kibali, wangefungua maombi kuiomba mahakama izifute kanuni hizo na kumzuia mjibu maombi wa kwanza (INEC) kuendelea na mchakato wa uchaguzi kwa kutumia kanuni hizo.

Katika ombi la nyongeza kupitia kanuni ya 5(6) za mapitio ya Mahakama kama ilivyotangazwa katika GN namba 324 ya 2014, waliomba kwamba kama maombi yao yatakubaliwa, basi kanuni hizo zisitumike hadi ombi lao lisikilizwe na kuamuliwa.

Wajibu maombi waliwasilisha kiapo kinzani kilichoapwa na Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa INEC, ambacho kilijibiwa na waombaji.

Katika usikilizwaji wa maombi, waombaji waliwakilishwa na mawakili Mpale Mpoki na Jebra Kambole, huku wajibu maombi wakiwakilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Mark Mulwambo, akisaidiana na mawakili Erigh Rumisha na Edwin Webiro.

### Hoja za wanaopinga kanuni

Kambole alijieleza mahakama kuwa wateja wake si tu wamewasilisha ombi hilo ndani ya muda wa miezi sita unaotakiwa na sheria, bali wana kesi yenye mashiko ambayo wana masilahi nayo.

Alisema waombaji wana masilahi ya kutosha katika maombi hayo kwa sababu wanaamini kuwa, kama wapigakura walioandikishwa wanaotarajia kupiga kura, wataathiriwa na kanuni hizo.

Ili kuishawishi Mahakama kuwa wana masilahi makubwa na maombi hayo, walijenga hoja sita zifuatazo:

Moja, maneno "washiriki wa uchaguzi" yaliyotumika katika utangulizi wa kanuni yanaulenga umma.

Pili, waombaji ni raia wa Tanzania wenye haki ya kupiga kura na kuchaguliwa.

Tatu, wao ni wapigakura walioandikishwa, hivyo wana haki ya kupiga kura na kuchaguliwa, na wana mpango wa kugombea.

Nne, wana masilahi na uchaguzi wa huru na haki katika nchi ya Tanzania.

Tano, wana masilahi kama wapigakura na haki ya kumchagua mgombea wanayemtaka katika uchaguzi huo. Sita, kanuni hizo zinaweka msingi wa haki na wajibu kwa wagombea, wanachama wa vyama vya siasa na wafuasi wao, hivyo wajibu huo ni

**SOMA ZAIDI**

**Aliomba Mahakama itupilie mbali maombi ya waombaji kupewa kibali cha kufungua maombi ya mapitio ya Mahakama kupinga kanuni hizo za maadili ya uchaguzi.**

**Awali, kabla ya kusikiliza maombi hayo, INEC na AG waliwasilisha pingamizi wakidai kuwa hati ya kiapo cha waleta maombi cha kuunga mkono ombi lao ilikuwa na dosari isiyoweza kutibika kwa kuwa na maoni, hoja na hitimisho kinyume cha sheria.**

**Baada ya mawasilisho ya hoja za mawakili wa pande zote mbili, Jaji alilikataa pingamizi hilo. Uamuzi huo uliwezesha kusikilizwa kwa maombi hayo ambayo yametupwa na Mahakama kwa kukosa mashiko.**

> **"Lengo la waombaji si kusimamisha mchakato wa uchaguzi bali kuiwezesha Mahakama kuangalia misingi ya kisheria ya kanuni hizo itakazo-simamia maadili, kwani kama wakishinda hawata-fidiwa.."**
>
> Wakili Mpoki



Scanned with MOBILE SCANNER

# Kesi ya Lissu yasubiri uamuzi Mahakama Kuu

**Na Ramla Hamidu**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeahirisha usikilizaji wa kesi ya kutoa taarifa za uongo na uchochezi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu.

Mahakama hiyo ilitoa uamuzi huo ikieleza kwamba itaendelea kusikiliza shauri hilo baada ya uamuzi wa maombi namba 14496/2025 na 15635/2025 yaliyopelekwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam masijala ndogo utakapotolewa.

Uamuzi huo ulitolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Geoffrey Mhini jana wakati shauri hilo namba 8606 liliposikilizwa mbele yake baada ya kufikishwa kwa ajili ya kuendelea na usikilizwaji.

Awali, Wakili wa Serikali Mkuu, Nassoro Katuga alidai shauri hilo lilipelekwa kwa ajili ya kusikilizwa lakini alidai kuna maombi ambayo upande wa mshitakiwa uliyapeleka mahakama kuu ambayo uamuzi utakaotolewa, utaathiri mwenendo wa shauri hilo.

Katuga alidai katika maombi namba 14496/2025 waliomba mapitio ya shauri hilo namba 8606/2025 hususani katika uamuzi wa mahakama hiyo kuahirisha shauri Juni 2, 2025 wakiomba Mahakama Kuu kutathmini uamuzi huo na kuufuta.

Alidai maombi hayo yalipelekwa kwa ajili ya kusikilizwa Juni 27, mwaka huu lakini hayajasikilizwa kwani mapingamizi yaliyowasilishwa na upande wa Jamhuri yalisikilizwa na yanatarajiwa kutolewa uamuzi Julai 11, mwaka huu.

Alidai Juni 26, mwaka huu upande wa mshitakiwa walipeleka maombi mengine na kusajiliwa kwa namba 15635 ambayo yapo kinyume na maombi namba 13298/2025 yaliyowasilishwa na jamhuri katika shauri la Mahakama Kisutu yaliyokuwa yakiomba kufichwa mashahidi.

Katuga alidai kuendelea na usikilizwaji kutafanya uamuzi uliotolewa awali na mahakama, kubaki ukining'inia. Alidai si busara kuendelea kabla ya uamuzi wa maombi hayo haujatolewa akisisitiza kwamba uamuzi wa maombi yote utaathiri shauri hilo na kuomba ahirisho.

Wakijibu hoja hizo, mawakili wa utetezi, Mpare Mpoki, Dk Rugemeleza Nshala na Peter Kibatala walidai hawakubaliani na ahirisho hilo. Waliomba mahakama iendelee na usikilizwaji.

Walidai kuwa maombi hayo yaliyopelekwa kabla ya Juni 16, mwaka huu, walianza kusikiliza shauri hilo na shahidi waliyekuwa wakimtegemea ni askari ambaye hawezi kuathiriwa na maombi ya Mahakama Kuu kwani si miongoni mwa mashahidi wa kificho.

Baada ya kuelezwa hayo, Hakimu Mhini alisema kutokana na hoja za pande zote mbili kuwa kwamba kuna maom[illegible]fungu[illegible]wa mahaka[illegible]u ambayo hayajatolew[illegible]uzi bado, hivyo rekodi za mahakama zitaathirika kutokana na uamuzi wa mahakama kuu.

Pia, alisema kwa sababu jalada limeshaitishwa Mahakama Kuu na hawezi kuendelea na kesi ambayo hana jalada lake, aliahirisha usikilizwaji wa shauri hilo hadi uamuzi wa Mahakama Kuu utakapotolewa.

Katika kesi hiyo, ilidaiwa Aprili 3, mwaka huu katika shitaka la kwanza Lissu alichapisha taarifa: "Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 wagombea wa Chadema walienguliwa kwa maelekezo ya Rais".

Katika shitaka la pili inadaiwa Aprili 3, mwaka huu Lissu kupitia mtandao wa Youtube alichapisha taarifa: "Mapolisi wanatumika kuiba kura wakiwa na vibegi".

Kwenye shitaka la tatu, Lissu anadaiwa kuchapisha taarifa ya uongo kwa nia ya kupotosha umma kupitia mtandao wa Youtube inayosema, "Majaji ni ma-CCM hawawezi kutenda haki, [illegible] kuchaguliwa kuwa majaji wa mahakama ya rufaa."